**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA RAIS
## MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Simu Na: +255 (026) 2963630
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: http://www.utumishi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P. 670,
**DODOMA.**

***Unapojibu tafadhali taja:***

Kumb. Na. CGB.53/472/01/"A"/80

09 Januari, 2025

Makatibu Wakuu,
Makatibu Tawala wa Mikoa,
Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma,
Wakuu wa Idara za Serikali Zinazojitegemea,
Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali,
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, na Miji,
Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya,
**TANZANIA BARA.**

Yah: **UTARATIBU WA UJAZAJI WA HATI YA AHADI YA UADILIFU (INTEGRITY PLEDGE) TOLEO LA MWAKA 2025 KWA WATUMISHI WA UMMA**

Tafadhali rejea barua yenye Kumb. Na. EG.45/86/01/"D"/48 ya tarehe 07 Oktoba, 2015 (nakala imeambatishwa) iliyotoa maelekezo ya utekelezaji wa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa watumishi wa umma PL. Na. 4.

2. Kufuatia mabadiliko yaliyofanyika katika miongozo ya kiutumishi ikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, pamoja na Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023, kumekuwepo na changamoto katika utekelezaji wa Hati ya Ahadi ya Uadilifu. Changamoto hiyo inatokana na hati zinazotumika sasa kurejea miongozo iliyopitwa na wakati.

3. Katika kuhakikisha Hati ya Ahadi ya Uadilifu inaakisi mahitaji ya sasa na mabadiliko ya Miongozo ya kiutumishi, Ofisi imehuisha Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma Toleo la Mwaka 2015 kuwa kutoa Toleo jipya la Mwaka 2025. Kwa msingi huo, mnaelekezwa kuhakikisha kuwa: -

(i) Watumishi wa Umma wote ambao hawako katika ngazi ya Uongozi, watakaojiriwa; kupandishwa vyeo; kubadilishwa kada; na kuhamia katika Taasisi zenu **kuanzia Januari 2025** Wanajaza Hati ya Ahadi ya Uadilifu Toleo la mwaka 2025 kupitia Fomu iliyopo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi);

(ii) Watumishi wa Umma wote ambao hawako katika ngazi ya Uongozi, walioajiriwa; kupandishwa vyeo; kubadilishwa kada; na kuhamia katika taasisi zenu **kabla ya Januari, 2025**, walijaza Hati ya Ahadi ya Uadilifu, Toleo la mwaka 2015; na

(iii) Taarifa ya taasisi ya utekelezaji wa Hati ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma inaandaliwa kwa kuzingatia **kiolezo** - "*format*" kilichoambatishwa na kuiwasilisha Ofisi ya Rais (UTUMISHI) ifikapo tarehe 31 Desemba, kila mwaka kupitia barua pepe ya **dep@utumishi.go.tz**.

4. Nawatakia utekelezaji mwema.

Xavier M. Daudi
**KAIMU KATIBU MKUU (UTUMISHI)**

***Kiambatisho A:***

## Kiolezo cha Taarifa ya Hati ya Ahadi ya Uadilifu

| "*Format*" kwenye "*Excel*": TAARIFA KUHUSU HATI YA AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA KWA KIPINDI HUSIKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JINA LA TAASISI:** | | | | |
| | | | | |
| 1 | IDADI YA WALIOPO KAZINI KUFIKIA TAREHE 31 DESEMBA, 2024 | IDADI YA WALIOJAZA KIAPO | IDADI YA AMBAO HAWAKUJAZA KIAPO | MAELEZO KUHUSU AMBAO HAWAKUJAZA |
| | 0 | 0 | 0 | |
| | | | | |
| 2 | IDADI YA WALIOAJIRIWA WAPYA KUANZIA 01, JANUARI, 2025 | IDADI YA WALIOJAZA KIAPO | IDADI YA AMBAO HAWAKUJAZA KIAPO | MAELEZO KUHUSU AMBAO HAWAKUJAZA |
| | 0 | 0 | 0 | |
| | | | | |
| 3 | IDADI YA WALIOHAMIA KUANZIA 01,JANUARI, 2025 | IDADI YA WALIOJAZA KIAPO | IDADI YA AMBAO HAWAKUJAZA KIAPO | MAELEZO KUHUSU AMBAO HAWAKUJAZA |
| | 0 | 0 | 0 | |
| | | | | |
| 4 | IDADI YA WALIOPANDA CHEO KUANZIA 01,JANUARI,2025 | IDADI YA WALIOJAZA KIAPO | IDADI YA AMBAO HAWAKUJAZA KIAPO | MAELEZO KUHUSU AMBAO HAWAKUJAZA |
| | 0 | 0 | 0 | |
| | | | | |
| 5 | IDADI YA WALIBADILISHIWA KADA KUANZIA 01, JANUARI, 2025 | IDADI YA WALIOJAZA KIAPO | IDADI YA AMBAO HAWAKUJAZA KIAPO | MAELEZO KUHUSU AMBAO HAWAKUJAZA |
| | 0 | 0 | 0 | |

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA
## HATI YA AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA
## (Kwa Utumishi wa Umma Uliotukuka)

**Kwa kutambua dhamira ya kuufanya utumishi wa umma kuwa wenye ufanisi na kuheshimika kutokana na watumishi kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298, Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Sura 309, Sheria ya Serikali Mtandao Sura 273, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023 pamoja na kuwa na mwenendo unaozingatia Maadili katika Utumishi wa Umma.**

**Mimi....................................................................................................................... ninaahidi kwa umma kwamba:-**

1. Nitakuwa Mzalendo kwa nchi yangu na mtii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Nitahudumia Umma na watumishi wenzangu kwa heshima na usawa bila kufanya ubaguzi kwa misingi ya dini, siasa, kabila,udugu, ukanda,jinsia, urafiki au hali ya mtu;
3. Nitatimiza wajibu wa kutoa huduma bora kwa umma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma;
4. Nitalinda na kutumia rasilimali za umma kwa manufaa ya Umma;
5. Nitafanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu;
6. Sitaomba, kushawishi, kutoa wala kupokea rushwa, zawadi au fadhila zilizokatazwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;
7. Sitatumia madaraka yangu kwa manufaa binafsi, ya ndugu, rafiki na jamaa zangu na nitajiepusha na mgongano wa maslahi;
8. Nitaepuka tabia ambayo inavunja heshima ya Utumishi wa Umma na Serikali hata ninapokuwa nje ya mahali pa kazi;
9. Sitatoa Siri za Serikali au za mtejakwa watu wasiohusika isipokuwa kwa maslahi ya Umma;

**Tamko: Ninakiri kwamba nimeisoma na kuielewa Hati hii ya Ahadi ya Uadilifu kabla ya kuweka saini. Ninaelewa kwamba nina wajibu wa kuheshimu Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura 20, Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura 348, Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Sura 309, Sheria ya Serikali Mtandao Sura 273, Sheria za Kisekta na Sheria nyingine zote za nchi, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023, Kanuni za Maadili ya Kitaaluma na kwamba, endapo nitakiuka Sheria na Kanuni zilizotajwa, hatua za kinidhamu na kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yangu.**

| ............................................ | ................................. | ........................ | ...................... |
| --- | --- | --- | --- |
| JINA | CHEO | SAINI | TAREHE |
| ............................................ | ................................. | ........................ | ...................... |
| MTENDAJI MKUU WA TAASISI | TAASISI | SAINI | TAREHE |